# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA PROF. ANNA KAJUMULO TIBAIJUKA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

## DIRA YA WIZARA:

Kuwa na uhakika wa miliki za ardhi, nyumba bora na makazi endelevu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

## DHIMA:

Kuweka mazingira yanayofaa kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi, nyumba na makazi.

## MAJUKUMU:

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inayo majukumu yafuatayo:-

i. Kuandaa sera na mikakati ya uendelezaji wa sekta ya ardhi;
ii. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi;
iii. Kusimamia upangaji wa miji na vijiji;
iv. Kupima ardhi na kutayarisha ramani;
v. Kutoa hati za kumiliki ardhi na hatimiliki za kimila;
vi. Kusajili hati za umiliki ardhi na nyaraka za kisheria;
vii. Kuthamini mali;
viii. Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwa na nyumba bora;
ix. Kutatua migogoro ya ardhi na nyumba;

x. Kusimamia upatikanaji na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
xi. Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na huduma za sekta ya ardhi;
xii. Kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi na Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni;
xiii. Kusimamia uendeshaji wa Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro; na,
xiv. Kusimamia maslahi na utendaji kazi wa watumishi wa sekta ya ardhi.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, Mpango Mkakati wa Wizara (2012/13-2016/17), Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na miongozo mbalimbali ya Serikali.

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA PROF. ANNA KAJUMULO TIBAIJUKA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2012/13 na malengo ya Wizara katika bajeti ya mwaka 2013/14. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/14.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Waheshimiwa Wabunge kuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano wa kumi na moja wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Pia, ninampongeza Mheshimiwa James Daudi Lembeli (Mb), Mwenyekiti, na Mheshimiwa Abdulkarim E. Hassan Shah (Mb), Makamu Mwenyekiti kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Aidha, nawapongeza wajumbe walioteuliwa kwenye kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mbunge wa Peramiho) na Mussa Zungu Azzan (Mbunge wa Ilala) kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Wenyeviti wa Bunge.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa aipokee na kuilaza pema roho ya Marehemu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani. Vilevile, kwa namna ya pekee natoa pole kwa Watanzania wenzangu walioathirika na majanga mbalimbali likiwemo la kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 Jijini Dar es Salaam.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** pili, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya

Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais; na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa, ulioniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; pia, Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Mhe. Balozi Ali Idd Seif, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nakupongeza wewe kwa umahiri na umakini ambao umeonesha katika kuongoza shughuli za Bunge. Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza na kukupa nguvu, afya na hekima za kumudu zaidi majukumu yako. Pia nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge wa Kongwa) na Naibu Spika wa Bunge letu kwa utendaji mzuri katika kuendesha shughuli za Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao. Pamoja na kuwa na kazi nyingi za kitaifa, wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini wamekuwa wakinipa ushirikiano mzuri na kujitahidi kukutana nami ninapopata nafasi kufika jimboni kwa kuhudhuria vikao na mikutano katika tarafa zao au kupokea wageni na wataalaam waelekezi ninaowatuma kufika kusukuma maendeleo yetu. Ninawashukuru sana kwa uelewa na ushirikiano, na uongozi madhubuti wa madiwani na wenyeviti wa vijiji kuunda Mifuko ya Maendeleo ya Kata ambayo italeta mapinduzi katika kupunguza umaskini na kutuletea maendeleo endelevu. Ninawapongeza Madiwani ambao tayari wamesajili taasisi ya mifuko hiyo katika kata za Mubunda, Kyebitembe, Rulanda, Muleba, Bureza, Magata, Karutanga, Kimwani, Mazinga, Nyakabango, Nshamba, Kishanda, Buganguzi, Burungura, Buhangaza, Kashasha, Ijumbi na Muleba Mjini. Ninawahimiza wale ambao bado hawajakamilisha zoezi hili wakazane tusonge mbele kwa pamoja. Aidha, ninawashukuru ndugu, jamaa na marafiki walionisaidia na kunipa ushirikiano wa karibu katika kutimiza

majukumu ya Uwaziri na Ubunge. Nawashukuru wananchi na kuwahakikishia popote pale mlipo, iwe Tarafa ya Nshamba, Kimwani au Muleba yenyewe, kwamba tutayalinda mafanikio tuliyoyafikia na kuongeza kasi zaidi ili kufikia malengo ya kulinda amani, utulivu na kufikia maisha bora. Namuomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kila mwananchi kulitambua hili na kuchangia katika nafasi yake kwa kadri ya uwezo wake kufikia maisha bora. Mwisho ninatuma salamu kwa mama yangu mzazi Ma Aulelia Kajumulo hapo Muleba. Sala zake za kila siku anapokuwa na nguvu zinasikika maana huku mie ni mzima wa afya.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ambao wamenisaidia katika kutekeleza majukumu yangu magumu hasa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi sehemu mbalimbali nchini, na wale walioniamini na kunichagua kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Kamati yake Kuu. Hii imenipa nguvu mpya katika kutekeleza ilani ya CCM. Pia ninawashukuru, viongozi na watendaji wa Serikali kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Aidha sina budi

kutambua mchango wa viongozi wa dini na vyama vya hiari ambao nimeshirikiana nao katika kazi zangu za kutatua migororo na changamoto nyingi za sekta ya ardhi ambazo zinahitaji ushiriki wao.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli (Mbunge wa Kahama), kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Natoa shukurani za pekee kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye (Mbunge wa Arumeru Magharibi) kwa ushirikiano na umoja tuliojenga kutekeleza majukumu yetu. Nawashukuru pia Katibu Mkuu Bw. Patrick Rutabanzibwa; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Maria Bilia; watendaji katika Idara, Vitengo, Shirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushauri na mshikamano wao katika kupanga na kutekeleza mipango ya Wizara. Zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta yetu lakini kwa mshikamano na umoja naamini tutaweza kukabiliana nazo.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA ARDHI**

9. **Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba yangu ya Bajeti mwaka juzi na mwaka jana, nilichukua muda mrefu kulieleza Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla, changamoto muhimu zinazokabili Sekta ya Ardhi na kuziorodhesha kwa urahisi wa rejea. Vilevile, nilieleza na kufafanua hatua zilizokuwa zinachukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto hizo. Kwa kifupi, changamoto hizo zinagawanyika katika maeneo manne (4) makubwa kama ifuatavyo:

i. uelewa usiotosheleza wa wananchi kuhusu sekta yenyewe hasa sheria zake na miongozo iliyopo; haki zao pamoja na wajibu wao;

ii. nafasi ya vyombo mbalimbali vya usimamizi na utendaji wake;

iii. vitendea kazi vilivyopo na vinavyohitajika ili kukidhi mahitaji ya sekta nyeti ya ardhi ambayo ni kiungo muhimu katika maendeleo; na,

iv. mazingira ya utendaji yaliyoko nje ya uwezo wa Wizara.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kuwa kutokana na maumbile ya changamoto

zenyewe, mwaka mmoja ni muda mfupi mno kuweza kutoa tathmini kamili ya utekelezaji kwani juhudi za kukabiliana na changamoto nyingi huchukua muda ili matokeo yake yaweze kupimika kwa usahihi. Tumepanga kutoa tathmini kamili mwaka kesho ambapo itakuwa ni miaka mitatu ya utekelezaji tangu nilipopewa dhamana ya kusimamia sekta hii nyeti na mtambuka katika taifa letu. Katika hotuba hii, nitaeleza kwa kifupi tu mwelekeo na matokeo ya awali ya utekelezaji, changamoto mpya zinazojitokeza, na hatua zinazochukuliwa.

11. ***Mheshimiwa Spika***, ninayo furaha kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na changamoto hizo, tumepiga hatua muhimu na kuongeza matumaini kwa Watanzania walio wengi kuhusu Serikali kuwajali na kutetea haki zao za ardhi na kuweka misingi ya kuwawezesha kuwa na nyumba na makazi bora. Upo ushahidi kuwa uelewa umeongezeka kwani wengi sasa wanajitokeza kudai haki zao bila woga, na wananchi wengi pamoja na taasisi mbalimbali zimetoa ushirikiano hata kusababisha baadhi ya malengo kuvukwa. Matokeo yake ni kwamba kinachosababisha kasi ndogo katika utekelezaji wa baadhi ya malengo, kama

itakavyodhihirika mwaka 2012/13 ni uwezo mdogo wa utekelezaji kwa maana ya Bajeti finyu, utaalam unaohitaji kukuzwa na nyenzo za utekelezaji zinazohitaji kuongezwa na kuboreshwa. Hii ndiyo maana **kauli mbiu** ya Wizara katika mwaka wa 2013/14 ni '***Kuendeleza Sekta ya Ardhi, kama kichocheo cha maendeleo na silaha ya kuondoa umaskini.***'

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza hayo, naomba sasa nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango wa Wizara wa Mwaka 2012/13 na Shabaha za Mpango wa Mwaka 2013/14. Napenda kutoa angalizo kuwa takwimu nyingi za utekelezaji zinaishia Mwezi Aprili, 2013 na huenda zitakuwa tofauti ifikapo mwisho wa Mwezi Juni, 2013.

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2012/13 NA MALENGO YA MWAKA 2013/14

## Ukusanyaji wa Mapato

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 99.8 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika sekta ya ardhi. Hadi Aprili, 2013 jumla ya Shilingi bilioni 19.1 zilikusanywa. Upungufu huu ulitokana na changamoto mbalimbali ikiwepo kuchelewa kuanza kutumika kwa viwango vipya vya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara imeweka lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 100.** Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatavyo: kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi; kupanga, kupima na kumilikisha maeneo mapya; kukamilisha upimaji na umilikishaji wa viwanja kwenye maeneo ambayo upimaji wake haujakamilika; kuhamasisha wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi; kutuma ankara za madai kwa kutumia simu za kiganjani; kutumia kampuni binafsi kukusanya kodi na

kuwachukulia hatua za kisheria wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi. **Nitumie fursa hii kuwakumbusha wananchi kutimiza masharti ya umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi, ada na tozo nyingine kwa mujibu wa sheria. Wizara yangu inaziagiza Halmashauri zote nchini kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wote ambao hawajalipa kodi ya pango la ardhi ikiwa ni pamoja na kufuta milki zao na kuwafikisha mahakamani. Aidha, tutachukua hatua dhidi ya waliojimilikisha maeneo makubwa ya ardhi vijijini zaidi ya ekari 50 lakini kukataa kutafuta hatimiliki kwa hiyo kuendelea kutoyalipia kodi ya ardhi maeneo hayo. Kwa sasa hivi kodi ya ardhi haitozwi kwa ardhi yote isiyokuwa na hatimiliki ya kawaida**

**Matumizi**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 101.7**. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 10.4** sawa na asilimia **10.25** ya fedha zilizoidhinishwa zilitengwa kwa ajili ya mishahara; **Shilingi bilioni 20.3** sawa na

asilimia **19.96** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo; na **Shilingi bilioni 71** sawa na asilimia **69.79** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 61** ni za ndani na **Shilingi bilioni 10** ni za nje. Hadi Aprili, 2013 jumla ya fedha zilizotolewa ni **Shilingi bilioni 34.42** sawa na asilimia **33.83** ya fedha zilizoidhinishwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 24.57** sawa na asilimia **71.39** ya kiasi kilichotolewa, zilitumika (**Jedwali Na. 1**). Matarajio ya wizara ni kuwa hadi Juni, 2013 kiasi kikubwa cha fedha kilichoidhinishwa kitatolewa na kutumika hasa ikizingatiwa kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya fedha iliyobaki ni kwa ajili ya ulipaji wa fidia.

## UTAWALA WA ARDHI

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika hotuba yangu ya mwaka jana, nilieleza kwa kirefu kuhusu ngazi tatu muhimu zinazotambulika kisheria katika kugawa na kusimamia ardhi. Ngazi hizo ni Kijiji, Halmashauri ya Wilaya au Mji na Taifa chini ya Kamishna wa Ardhi. Napenda kukiri kuwa katika mwaka huu unaokwisha, japokuwa uelewa wa nafasi na majukumu ya ngazi hizi umeendelea kuwa mzuri, idadi ya malalamiko bado iko juu, kwa

kutumia kigezo cha walalamikaji ambao bado wanafika Wizarani badala ya kutatua matatizo yao katika ngazi husika.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** migongano inayotokea kwa kutokufuata kanuni ina gharama kubwa kwa wahusika, huchelewesha maendeleo na kudhoofisha dhamira ya Serikali ya kufanya ardhí kuwa kichocheo cha maendeleo na nyenzo muhimu katika kupambana na umaskini. **Ninasisitiza tena kuwa wahusika wote wapitie miongozo iliyopo kwa makini ili kuepusha migongano isiyo ya lazima**.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Mgawanyo huo bado haubadili ukweli kwamba mhimili mkuu wa Sekta ya Ardhi ni Wizara yenyewe kwani yapo majukumu ambayo ni lazima yatekelezwe na Wizara yenyewe. Kuhusu majukumu hayo, na ili kupunguza msongamano Wizarani na kusogeza huduma hizo karibu na wananchi, uanzishwaji wa Ofisi za Ardhi za Kanda sasa umekamilika. Wananchi waelekeze hoja zao katika ofisi hizo.

**Ofisi za Ardhi za Kanda**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka

2012/13, Wizara yangu iliahidi kuanza kutoa huduma za ardhi katika Ofisi ya Ardhi ya Kanda ya Magharibi iliyopo mjini Tabora. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wizara iko katika hatua za mwisho kuhakikisha kuwa ofisi hiyo itaanza kutoa huduma kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2012/13. Kanda hii inahudumia mikoa ya Tabora, Katavi, Shinyanga na Kigoma ambayo awali ilikuwa inahudumiwa na Kanda za Ziwa (Mwanza) na Kusini Magharibi (Mbeya). Ni matumaini yangu kwamba kwa hatua hii, matatizo ya wananchi wengi yataweza kutatuliwa kwa wepesi na haraka zaidi. Hili nalo limeongeza changamoto kwa Wizara ambayo itahakikisha kuwa ofisi hizi zinapewa wafanyakazi na vifaa vya kutosha ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Na.4 na Na.5 ya Mwaka 1999**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** sheria za ardhi Na. 4 na Na. 5 za mwaka 1999 zinatoa miongozo muhimu ya kumiliki ardhi Tanzania. Sheria hizi zinatoa fursa ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inamilikiwa kisheria. Wananchi wengi wamejitokeza kupata hatimiliki, wakati mwingine hata kupita uwezo uliopo wa

kutimiza maombi yao kwa haraka wanayotarajia. Wizara inaendeleza jitihada za kuhakikisha kuwa hatimiliki hizi zinapatikana haraka kwa wanaostahili kama sehemu muhimu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kuwa kuwapo kwa ardhi ya kutosha Tanzania pia kumeibua changamoto nyingine. Wageni wengi, hasa kutoka nchi jirani wameendelea kujaribu kujipenyeza ili kumiliki ardhi kwa njia za udanganyifu na mara nyingine wakisaidiwa na baadhi ya wananchi na hata viongozi waliopoteza maadili. Nilikemea tabia hiyo mwaka jana na kueleza kwa kirefu njia sahihi ya kuwahudumia wageni wenye nia ya kupata ardhi Tanzania. **Ninarudia kusisitiza kuwa wenye tabia hiyo waiache mara moja maana wakibainika, hawatavumiliwa kamwe na sheria itachukua mkondo wake**.

**Utoaji Milki za Kawaida, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kutayarisha na kutoa

hatimiliki za kawaida **40,000**. Hadi kufikia Aprili, 2013 Wizara ilitoa hatimiliki **21,846** sawa na asilimia **54.62** ya lengo (**Jedwali Na.2)**. Kwa mwaka 2013/14 Wizara imepanga kutoa hatimiliki 40,000**. Napenda kurudia wito wangu kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa hati ili wananchi waweze kuwa na miliki salama.**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kushughulikia maombi ya uhamisho 1,700, na kufikia Aprili, 2013 maombi 672 yameshughulikiwa. Kwa mwaka 2013/14 wizara itashughulikia maombi ya uhamisho wa milki **1,800**. Vilevile katika kutekeleza jukumu la Wizara la kusimamia masharti ya umiliki wa ardhi na kuhakikisha kuwa inaendelezwa ipasavyo, hadi kufikia Aprili, 2013 ilani za ubatilisho **3,053** zilitumwa kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki. Aidha, kwa mwaka 2013/14, Wizara inakusudia kushughulikia **ubatilisho wa milki zote zinazokiuka masharti ya uendelezaji wa viwanja na mashamba ili ardhi iliyomilikishwa itumike kwa malengo yaliyokusudiwa.**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wananchi, kuhakiki mashamba, kuratibu utoaji vyeti vya ardhi ya kijiji na hati za hakimiliki ya kimila. Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji unaviwezesha vijiji kutambua maeneo yao kiutawala na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2012/13 Wizara iliweka lengo la kutoa Vyeti **2,007** vya Ardhi ya Kijiji lakini hadi Aprili, 2013 Wizara ilitoa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji **469.** Kutokufikiwa kwa lengo hili la utoaji wa vyeti vya Ardhi ya vijiji kunatokana na mabadiliko ya mipaka ya vijiji inayolazimu upimaji wa mipaka ya vijiji kurudiwa, na wakati mwingine migogoro kuhusu mipaka hiyo kuibuka na kuchelewesha upimaji. Katika kipindi hicho, Wizara iliratibu uandaaji, usajili na utoaji wa Hati za Hakimilki ya Kimila **32,155** katika Halmashauri za Wilaya ikilinganishwa na lengo la kutoa Hatimilki za Kimila **50,000.** Pia, Masjala za Ardhi **122** zilianzishwa (**Jedwali Na. 3**). Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya nchini pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba zoezi

la utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila linakuwa endelevu.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/14, Wizara itaendelea na utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na kuhamasisha Halmashauri za Wilaya 28 zilizo kwenye maeneo ya ukanda wa SAGCOT (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania) kuanzisha mchakato wa uhakiki wa maslahi katika ardhi ya kijiji na utoaji wa Hati za Hakimilki za Kimila. Pia, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Halmashauri za Wilaya, na wadau wengine itaendelea kuratibu utayarishaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **50,000** nchini. Mfano, wananchi wenye hati hizo katika Halmashauri za Wilaya za Mbozi na Ileje wameweza kupata mikopo kwa kutumia hati hizo yenye jumla ya shilingi bilioni 26 kutoka Benki za CRDB, Stanbic, NMB, Mwananchi na Mfuko wa Pembejeo. **Natoa rai kwa wananchi washirikiane na Halmashauri zao kuhakiki na kupima maeneo yao na kupata Hati za Hakimiliki za Kimila, kwani hati hizi zina umuhimu mkubwa ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kuzitumia kama dhamana**

**ya mikopo kwenye taasisi za kifedha na kuepusha migogoro ya ardhi. Sina budi kuzishukuru benki ambazo zimetambua kwamba hatimiliki za kimila zinaweza kutumika kuchukua mikopo. Hapohapo ninahimiza benki na taasisi nyingine za fedha kutoa ushirikiano na kutambua kwamba hatimiliki za kimila zina nguvu ya kisheria katika kutumika kama dhamana. Hii itapunguza adha kwa wananchi wengi kulazimika kutafuta hatimiliki za kawaida ili kupata mikopo, jambo ambalo ni gumu zaidi maana linahitaji kwanza ardhi za vijiji kuhaulishwa na Mhe Rais kabla hati kama hizo kutolewa.**

**Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria**

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2012/13 Wizara yangu ilikuwa na lengo la kusajili Hati za kumiliki ardhi pamoja na Nyaraka za kisheria zipatazo **75,000,** kati ya hizo **35,000** ni hatimiliki na **40,000** zilikuwa ni Nyaraka za Kisheria. Hadi kufikia Aprili, 2013 hatimiliki na nyaraka za kisheria zipatazo **61,083** zilisajiliwa sawa na asilimia **81.4.** Kati ya hizo hatimiliki ni **24,421** pamoja na nyaraka zipatazo **28,407** zilisajiliwa chini

ya Sheria ya Usajili wa Ardhi Sura Na. 334 (**Jedwali Na. 4a**). Aidha nyaraka **7,305** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura Na. 117 (**Jedwali Na. 4b**). Vilevile, rehani za mali zinazohamishika zipatazo **950** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika Sura Na. 210.

28. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2013/14, Wizara ina lengo la kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria **80,000** na kati ya hizo **35,000** ni hatimiliki ambapo **45,000** ni nyaraka za kisheria.

**Kuboresha Kumbukumbu za Ardhi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji miliki mbalimbali ni hatua moja muhimu lakini uwezo wa kuzitambua kwa haraka na kuzisimamia ipasavyo ni muhimu zaidi. Katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013 niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ingeweka na kuhuisha mfumo wa kutunza kumbukumbu za walipa kodi ya ardhi wa *Land Rent Management System* (LRMS) katika ofisi za Ardhi za halmashauri **30**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi kufikia Aprili

2013, Wizara yangu imefanikiwa kuhuisha na kuboresha mfumo wa LRMS katika Ofisi za ardhi katika halmashauri **35** (**Jedwali Na.5a**). Vilevile, kwa halmashauri 35 zilizowekewa mfumo huo, watumishi katika ofisi zao za ardhi walipatiwa mafunzo.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara pia iliahidi kuendelea na kazi ya kuweka mfumo wa *Integrated Land Management Information System* (ILMIS). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hatua ya kwanza iliyohusu ubunifu wa mfumo imekamilika. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaanza hatua ya pili ya kuweka mfumo huo kwa awamu. Mfumo huo utakapokamilika, utaanza kutumika Makao makuu na hatimaye Ofisi za Ardhi za Kanda na Halmashauri zote.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara itaendelea na kazi ya kusimika mfumo wa kutunza kumbukumbu na kukadiria kodi ya ardhi (*Land Rent Management System* - LRMS *web based*) katika Ofisi za ardhi katika halmashauri **20** na kuboresha mfumo wa kumbukumbu za ardhi na kukadiria kodi katika ofisi za ardhi katika halmashauri **20** (**Jedwali 5b**).

## UTHAMINI WA MALI

32. ***Mheshimiwa* Spika**, Wizara yangu inaendelea kutekeleza jukumu lake la kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika kwa madhumuni mbalimbali. Madhumuni hayo ni pamoja na kuwezesha utozaji ushuru wa Serikali kutokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, mizania, kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi. Pia, wizara inasimamia utendaji wa taaluma ya uthamini nchini.

**Uthamini wa Ujumla/Kawaida**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya mwaka 2012/13, niliahidi kuwa Wizara itathamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **14,000** kwa madhumuni mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, hadi Aprili 2013, Wizara ilifanya uthamini wa kawaida wa jumla ya mali **822** na kuidhinisha jumla ya taarifa za uthamini **7,510** zilizowasilishwa na kampuni binafsi za uthamini na Halmashauri mbalimbali nchini. (**Jedwali Na. 6a).** Kwa

mwaka 2013/14, Wizara yangu inalenga kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali **15,000** kwa matumizi mbalimbali kadri maombi yatakavyowasilishwa Wizarani.

**Uthamini wa Kisheria**

34. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mujibu wa sheria za ardhi Na.4 na Na.5 za mwaka 1999, ardhi ya mwananchi inapochukuliwa na Serikali kwa ajili ya miradi ya umma, mwananchi huyo anastahili kulipwa fidia ya haki, kamilifu na kwa wakati. Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu iliweka lengo la kufanya na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali za wananchi wapatao **15,000**. Hadi kufikia Aprili, 2013, mali za wananchi wapatao **32,484** ambao maeneo yao yaliguswa na miradi mbalimbali nchini zilithaminiwa. Miradi hiyo iliyotekelezwa kwa mwaka 2012/13 ni pamoja na uwekezaji kwenye migodi, kilimo, viwanda na vituo vya biashara. Pia utekelezaji wa mipango ya miji kwa ajili ya upimaji wa viwanja vya matumizi mbalimbali nchini; utekelezaji wa miradi ya barabara chini ya TANROADS; miradi ya maji na umeme; ujenzi wa shule, vyuo na hospitali; upanuzi wa viwanja vya ndege na maeneo ya huduma za jamii. Idadi ya walioguswa na kufanyiwa

uthamini kwenye kila Wilaya imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 6b.**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara inalenga kufanya uthamini wa mali za wananchi wapatao **40,000** kwa lengo la kulipa fidia katika miradi mbalimbali itakayotekelezwa nchini ukiwemo mradi wa kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni Wilaya ya Temeke, Jijini Dar es Salaam.

**Viwango vya thamani**

36. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kusimamia taaluma ya uthamini, Wizara yangu imeendelea kuhakikisha kuwa viwango vya bei ya soko kwa ajili ya ukadiriaji thamani ya ardhi na mazao kwa usahihi vinakuwepo. Kazi hiyo inalenga kujenga Hazina ya Takwimu za Uthamini (*Valuation Data Bank).* Katika mwaka 2012/13, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya iliweza kuandaa viwango vya awali vya thamani ya ardhi na mazao vya wilaya zote nchini. Majedwali hayo ya viwango vya awali pamoja na mwongozo wa jinsi ya kuendesha zoezi hilo vilisambazwa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kwa ajili ya kuanza kuvitumia.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendeleza zoezi la kuhakiki na kufanya uchambuzi wa viwango vya awali vinavyoendelea kutumika sambamba na kuweka utaratibu endelevu wa uhuishaji wa viwango vya thamani. Hii ni kutokana na ukweli kuwa thamani ya ardhi na majengo hubadilika kwa mujibu wa mwenendo wa nguvu ya soko na kadri miaka inavyopita. Aidha, Wizara yangu kwa kushauriana na Halmashauri itaendeleza mkakati wa kuwajengea wathamini uwezo ili kuimarisha ushiriki wao katika zoezi la kukusanya na kuchambua takwimu za viwango vya thamani kwenye maeneo yao kwa lengo la kujenga Hazina ya Takwimu za viwango vya thamani vya soko. Hatua hii ikitekelezwa kikamilifu, itaondoa au kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro inayotokea baada ya kukamilisha uthamini. **Hivyo, nazidi kusisitiza Halmashauri zote nchini kuwezesha zoezi endelevu la ukusanyaji takwimu za viwango vya soko vya thamani katika maeneo yao.**

**Kuanzishwa kwa Hazina ya Ardhi (*Land Bank*)**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kuanzisha chombo kwa ajili ya kusimamia Hazina ya Ardhi na kuanzisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutekeleza ahadi hii. Taratibu zitakapokamilika tutawasilisha muswada wa sheria ya kuanzisha rasmi vyombo hivyo. **Ninarudia kuliomba Bunge lako Tukufu kuendelea kuunga mkono utaratibu mpya wa kutoa ardhi kwa wawekezaji kwa msingi wa kugawana hisa utakaofuta taratibu zinazotumiwa na Halmashauri na Vijiji kwa sasa za kupewa gawio lisilozingatia misingi ya kiuchumi, kwa mfano wawekezaji kutoa zawadi ndogondogo kama visima vya maji, madarasa, barabara za vumbi na zahanati.**

## MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

39. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2012/13 Wizara yangu iliahidi kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya sita (6) za Ngorongoro, Tunduru, Mpanda, Muleba, Karagwe na Kyela. Pia, iliahidi kwamba Mabaraza matatu (3) katika

Wilaya za Nzega, Kilosa na Manyoni yataanza kufanya kazi. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mabaraza ya Nzega, Kilosa na Manyoni yameanza kufanya kazi. Aidha, Wizara yangu imeunda Mabaraza saba (7) katika Wilaya sita (6) nilizokuwa nimeahidi pamoja na Wilaya ya Ngara ambayo inaonekana kuwa na migogoro mingi na wananchi wanasafiri umbali mrefu kwenda Bukoba lilipo Baraza sasa. Taratibu za ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani na vitendea kazi zinaendelea ili Mabaraza haya yaweze kuanza kufanya kazi katika mwaka 2013/14. Aidha, Wizara yangu inakusudia kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya tano (5) za Kilindi, Mbulu, Kahama, Sengerema na Kasulu kwa lengo la kusogeza huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi karibu na wananchi. **Ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya husika ambao wameonyesha ushirikiano mzuri wa kuhakikisha kuwa Mabaraza haya yanaundwa kwa kutoa majengo yatakayotumika kama ofisi.**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kuimarisha Mabaraza ya Ardhi na

Nyumba ya Wilaya ambapo Mabaraza ya Kinondoni, Mwanza na Ilala yamepatiwa ofisi zenye kutosheleza mahitaji ili kuondoa msongamano. Aidha, ukarabati wa ofisi za Mabaraza ya Mbeya na Rukwa utakamilika katika mwaka 2012/13. Kadhalika, jumla ya kompyuta ishirini na moja (21) zimenunuliwa na kusambazwa ili kuongeza ufanisi wa kazi katika Mabaraza.
Wizara inakusudia kuboresha na kuimarisha Mabaraza haya kwa kuyapatia watumishi na vitendea kazi ili migogoro iweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka. Pia, Wizara itasambaza nakala za Kanuni za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za mwaka 2003 ambazo zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuwaelimisha wananchi kuhusu namna wanavyoweza kupata haki zao kupitia Mabaraza hayo.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya iliendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro. Hadi mwezi Juni, 2012 kulikuwa na jumla ya mashauri **17,654** na kuanzia mwezi Julai, 2012 jumla ya mashauri **12,074** yamefunguliwa. Katika mwaka wa fedha 2012/13 jumla ya mashauri **9,831** yameamuliwa na mashauri **19,897** yaliyobaki

na yatakayofunguliwa yataendelea kusikilizwa katika mwaka 2013/14 (**Jedwali Na.7**). Ongezeko la mashauri hayo kunachangiwa na utendaji hafifu usioridhisha wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata. **Natoa wito kwa Halmashauri zote kuimarisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata kwa kuyajengea uwezo ili yaweze kutatua migogoro kwa ufanisi na kwa haraka na hivyo kupunguza msongamano wa mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeshughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya utendaji wa kazi usioridhisha wa baadhi ya Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuchukua hatua mbalimbali kulingana na sheria na kanuni. Wizara inaendelea kufuatilia utendaji wa kazi wa Wenyeviti ili kuhakikisha kuwa wanajiepusha na matendo ambayo ni kinyume cha Sheria na Maadili ya kazi zao.

## HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

43. ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake

ya upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima. Ramani hizo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya matumizi kwa sekta mbalimbali.

**Utayarishaji Ramani**

44. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2012/13 Wizara yangu iliahidi kujenga na kuimarisha kanzi ya taarifa za kijiografia (*geo-database*). Kazi hiyo imeanza kwa kuchambua na kuziingiza kwenye kanzi ya taarifa za kijiografia za wilaya mpya kumi na tisa (19) katika mikoa mipya minne (4) ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Katika mwaka 2013/14 Wizara yangu itakamilisha kazi hiyo katika mikoa minne na itaendelea katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara. Pia, Wizara itakamilisha ufungaji wa mtambo mpya wa uchapishaji ramani ili kuhakikisha kuwa ramani zenye viwango stahiki zinapatikana kwa watumiaji mbalimbali.

**Mipaka ya Ndani ya Nchi**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** migogoro ya mipaka inaongezeka katika maeneo ya kiutawala hasa kati ya Wilaya na Wilaya na

hifadhi za Taifa na maeneo ya vijiji. Suluhisho kwa migogoro hii ni kuhakiki na kupima maeneo hayo ili mipaka sahihi iweze kujulikana. Katika mwaka 2012/13 niliahidi kuwa Wizara itaboresha mfumo wa taarifa za kijiografia ili kutafsiri Matangazo ya Serikali yanayoainisha mipaka ya kiutawala ndani ya nchi lengo likiwa ni kuhakikisha mipaka hiyo inaeleweka kwa wahusika. Hadi Aprili 2013, Wizara yangu ilihakiki mipaka katika Wilaya za Meru (Mkoa wa Arusha) na Siha (Mkoa wa Kilimanjaro). Vilevile, katika kuzuia migogoro kati ya hifadhi na vijiji, Wizara kwa kushirikiana na TANAPA pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, inaendelea kuweka alama za kudumu za upimaji kwenye hifadhi ya Serengeti. Katika mwaka 2013/14 Wizara itaendelea na kutafsiri matangazo ya Serikali ya mipaka na kushughulikia migogoro ya ndani kwa kushirikisha wadau husika.

## Mipaka ya Kimataifa

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu ina jukumu la kuweka na kutunza alama za mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani. Katika mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kufanya mazungumzo na Burundi na kuimarisha alama za mpaka kati ya Tanzania na Kenya. Hadi Aprili, 2013 mazungumzo kati ya Tanzania na Burundi yamefanyika. Sambamba na mazungumzo hayo ukaguzi wa baadhi ya alama za mipaka ulifanyika na kubaini kuwa alama hizo ziko mbalimbali na nyingine zimeharibiwa. Alama zilizoharibiwa zitajengwa upya. Katika mwaka 2013/14, Wizara yangu imepanga kuimarisha mipaka 7 ya kimataifa ambayo ni kati ya Tanzania na nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Uganda na Kenya.

## Upimaji wa Mipaka ya Vijiji

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imekuwa ikiendelea na kazi ya upimaji wa mipaka ya vijiji. Katika mwaka 2012/13 Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya vijiji **200** ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 upimaji wa mipaka ya vijiji **216** ulikamilika katika Halmashauri za Wilaya za Bukoba

Vijijini (23), Urambo (50), Iringa Vijijini (24), Kilolo (23), Kilombero (53) na Ulanga (43). Kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji **100** katika wilaya za Songea, Tunduru, Nyasa, Namtumbo na Mbinga.

**Upimaji Viwanja na Mashamba**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2012/13 Wizara iliweka lengo la kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **40,000** na mashamba **1,000**. Hadi kufikia Aprili, 2013 Wizara yangu imeratibu na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **58,393** na mashamba **886**. (**Jedwali Na 8a**). Kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu imepanga kuratibu na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **60,000** na mashamba **1,000**.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kurahisiha upimaji wa ardhi na kupunguza gharama za upimaji kwa wananchi, katika mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kujenga vianzio vya upimaji (*Control Points*) **300** katika Miji **50**. Hadi kufikia Aprili, 2013 Wizara yangu imejenga alama **98** za vianzio vya upimaji katika Miji Saba ya Dar es Salaam (40), Kakonko (10), Kibondo (10), Musoma (9), Bukoba (10)

Mpanda (14) na Bariadi (5). Kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu itaendelea kusimika alama **300** katika miji **43** iliyobaki na miji mingine mipya saba. (**Jedwali Na. 8b**).

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusogeza huduma za upimaji ardhi karibu na wananchi Wizara yangu ina mpango wa kugatua mamlaka ya kusimamia kazi za upimaji ardhi katika ngazi ya Kanda. Lengo la uamuzi huu ni kusogeza huduma kwa wananchi na kupunguza gharama na muda wa Halmashauri.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kukabiliana na ongezeko la kumbukumbu za upimaji ardhi nchini, Wizara yangu imepanga kubadili kumbukumbu za upimaji ardhi kwenda katika mfumo kanzi wa kie-lektroniki (*Digital Cadastral Database*) na hatimaye kuziingiza katika mfumo unganishi wa kutunza kumbukumbu za ardhi. Hatua hii ni muhimu sana kwa kuwa itawezesha upatikanaji rahisi wa taarifa za ardhi na kuboresha utoaji wa huduma za upimaji ardhi nchini. **Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuboresha utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za Upimaji Ardhi ili kurahisisha upatikanaji wake.**

**Upimaji wa Ardhi chini ya Maji**

52. ***Mheshimiwa Spika****,* jukumu mojawapo la Wizara yangu ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonyesha umbile la ardhi chini ya maji hususan milima, mabonde miinuko na kina cha maji. Ramani hizi hutumika kuongozea vyombo vya majini, kubaini maeneo yanayofaa kwa bandari, kufanya tafiti mbalimbali na matumizi mengine. Katika mwaka 2012/13 Wizara ilipanga kununua kifaa cha upimaji majini kijulikanacho kama *echo sounder* ili kazi ya upimaji vina vifupi iweze kufanyika. Fedha kwa ajili ya ununuzi wa kifaa hiki zimetengwa katika mwaka 2013/14.

**Kuongeza eneo la ziada nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini (Extended Continental Shelf)**

53. ***Mheshimiwa Spika*****,** mwezi Agosti, 2012, Wizara yangu ilikamilisha na kuwasilisha andiko la kudai eneo la nyongeza nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini. Kukamilishwa kwa kazi hiyo kumeifanya Tanzania kuwa nchi ya 59 kuwasilisha andiko kwenye Umoja wa Mataifa, na hivyo kuwa kwenye orodha ya kusubiri mapendekezo ya Tume ya Mipaka ya

Umoja wa Mataifa ya kuitwa kwa ajili ya utetezi wa mwisho. Wizara yangu itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huu na kuteua wataalamu watakaoendelea na mradi huu hadi eneo linaloombwa litakapopatikana.

**Mfuko wa kupima Viwanja**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyolitaarifu Bunge hili mwaka 2012/13, Wizara yangu inaendelea kusimamia mfuko wa mzunguko wa kupima viwanja unaozipatia mikopo Halmashauri kwa ajili ya kulipa fidia, kupima viwanja na kumilikisha. Hadi Aprili, 2013 Halmashauri **26** bado hazijakamilisha urejeshaji wa mikopo hiyo yenye jumla ya Shilingi milioni **426.2** (**Jedwali Na. 9a**). Pia, Wizara imepokea maombi ya mikopo kutoka katika Halmashauri 12, na maombi hayo yanapitiwa ili mikopo ianze kutolewa. Kuhusu Halmashauri zilizokopa fedha kutoka kwenye mfuko wa mradi wa viwanja 20,000, Halmashauri nne hazijamaliza kurejesha mkopo huo wenye jumla ya **Shilingi bilioni 1.2** (**Jedwali Na. 9b**). Kuanzia mwezi Julai 2013, Wizara itakaa pamoja na halmashauri zinazodaiwa ili kuona namna nzuri ya kurejesha fedha hizo kwa haraka na hivyo

kuwezesha halmashauri zingine kunufaika na mikopo hiyo.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Wizara yangu kuendelea kufuatilia urejeshaji wa madeni hayo, Halmashauri sugu zinazodaiwa zitakatwa fedha zilizokopeshwa kutoka kwenye asilimia **30** ya fedha ambayo Halmashauri hurejeshewa baada ya makusanyo yake. Tunawasiliana na Wizara ya Fedha juu ya utekelezaji wa jambo hili ambalo limeathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa mfuko huu hasa kwa Halmashauri ndogo ambazo zingefaidika sana na huduma hii.

## MIPANGO MIJI NA VIJIJI

56. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi wa ustawi na maendeleo ya miji na vijiji hapa nchini ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu, ambayo yanaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendelezaji miji nchini.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Tanzania imeshuhudia ongezeko la watu na kasi ya ukuaji wa miji. Ongezeko hilo linajidhihirisha katika takwimu za sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya

mwaka 2012. Wakazi wa mijini waliongezeka kutoka **milioni 7.9** sawa na asilimia **23.1** mwaka 2002 hadi kufikia watu **milioni 12.7** sawa na asilimia **29.1** mwaka 2012**.** Inakadiriwa kwamba ifikapo mwaka 2025 asilimia **50** ya Watanzania watakuwa wanaishi mijini. Aidha, idadi ya miji imeongezeka kutoka Miji **31** mwaka 1957 hadi kufikia Miji **337** mwaka 2012.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** suala la ukuaji na ongezeko la miji sehemu nyingi duniani ni viashiria vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hapa nchini kumekuwa na changamoto nyingi zikiwemo Mamlaka za Miji kushindwa kumudu mahitaji ya nyumba na viwanja na kuweka huduma muhimu za kiuchumi na kijamii. Hali hiyo imesababisha wakazi wengi wa mijini kujenga holela. Inakadiriwa kwamba kati ya asilimia **60** na **75** ya wakazi mijini wanaishi katika maeneo yaliyoendelezwa holela.

**Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji Miji**

59. ***Mheshimiwa spika,*** katika kupanga Miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji huandaa

Mipango ya Jumla ya aina mbili ambayo ni; Mipango Kabambe ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji kwa muda mrefu wa miaka ishirini na Mipango ya Muda wa Kati ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji miji kwa muda wa miaka kumi.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha maandalizi ya rasimu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Bagamoyo imeandaa Mpango Kabambe wa Mji wa Bagamoyo. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia imeandaa Mpango wa Muda wa Kati wa Mji wa Kilindoni. Rasimu za awali za Mipango hiyo zimekamilika tayari kwa kuziwasilisha kwa wadau husika kuweza kupata maoni. Maandalizi ya Mpango wa Muda wa Kati wa Mji Mdogo wa Makambako na Mpango Kabambe wa Jiji la Mbeya yatafanyika baada ya kupata raslimali fedha.Kutokana na umuhimu wa miji kuwa na mipango ya Jumla wizara imewaandikia barua kuwataka Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zote kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya kuandaa Mipango hiyo.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia itakamilisha maandalizi ya Mpango wa Muda wa Kati wa Mji wa Kilindoni. Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Miji ya Mtwara, Njombe, Arusha, Sumbawanga, Bariadi na Mbeya ambazo ziliomba kujengewa uwezo wa kuandaa mipango ya jumla kwa ajili ya kuongoza na kusimamia ukuaji wa miji hiyo.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2012/13, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeendelea na uhamasishaji wa wadau katika ngazi mbalimbali, pamoja na ukusanyaji wa taarifa na takwimu muhimu ikiwa ni hatua ya awali ya uandaaji wa mpango wa uendelezaji upya eneo la Manzese. Vilevile wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza eneo la Makongo Juu kama eneo la mfano katika kuendeleza eneo na kudai tozo ya maboresho (*betterment fee*). Pia, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe, inaendelea kutayarisha mpango wa uendelezaji upya wa eneo la kati la mji huo. Kwa mwaka 2013/14 Wizara itaendelea

kushirikiana na Halmashauri husika kukamilisha na kutekeleza mipango hiyo.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu kwa kushirikiana na wizara ya Ujenzi imepata eneo huru kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayounganisha daraja la Kigamboni kwa upande wa Kurasini. Kazi hiyo imekamilika na ujenzi wa barabara na daraja la Kigamboni unaendelea. Pia, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara  zoezi la uthamini na ulipaji fidia wa eneo la ekari 60 lililotengwa kwa ajili ya kituo cha kimataifa cha kuratibu mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na China Kurasini linaendelea. Katika mwaka 2013/14, Wizara itaendelea kutafuta eneo huru la matumizi ya bandari na eneo la makazi mbadala huko Kigamboni Mtaa wa Kibada Uvumba kwa wale watakaohamishwa kutoka eneo la Kurasini.

**Urasimishaji Makazi Holela**

64. ***Mheshimiwa*** **Spika,** Katika mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kurasimisha makazi **4,000** katika Jiji la Mwanza. Hadi Aprili, 2013 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilikamilisha zoezi la urasimishaji wa makazi holela **1,970.** Vilevile elimu ya

urasimishaji na kuzuia makazi holela ilitolewa kwa wataalamu wa Halmashauri zilizoko katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Dodoma na Tabora.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/14 kazi ya kurasimisha makazi **2,000** katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza zitaendelea chini ya uratibu wa Wizara. Pia, Wizara itaendelea kutoa elimu ya urasimishaji kwa wataalam wa Halmashauri katika Kanda ya Nyanda za juu Kusini (Mbeya, Rukwa, Katavi na Iringa). **Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuweka mkazo katika suala la kupanga Miji na kusimamia kikamilifu Sheria za Mipangomiji na kanuni za ujenzi mijini ili kuzuia ujenzi holela.**

**Uendelezaji Miji Mipya na Vituo vya Huduma**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kuendeleza Kituo cha Huduma cha Luguruni. Wizara yangu imeteua Shirika la Nyumba la Taifa kuwa Mwendelezaji Mkuu wa kituo hicho na uendelezaji utaanza katika mwaka wa fedha 2013/14. Pia, Wizara

kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa nchini itaendelea kuainisha maeneo kwa ajili ya uanzishaji wa vituo vya huduma (*Miji ya Pembezoni*). **Natoa rai kwa Halmashauri za Manispaa na miji inayokua kwa kasi kuainisha na kuendeleza vituo vya huduma pembezoni mwa miji hiyo.**

**Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara yangu imeanza kazi ya uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni kwa kutekeleza kazi zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Wizara imeunda Wakala wa Kusimamia Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni *Kigamboni Development Agency* (KDA), ambayo ni Mamlaka ya Upangaji (*Planning Authority*) wa eneo la Mji Mpya Kigamboni lenye kata tisa ambazo ni Kigamboni, Tungi, Vijibweni, Mjimwema, Kibada, Somangila, Kisarawe II, Kimbiji na Pemba Mnazi.

***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuandaa michoro ya kina inayoonesha miundombinu inayotakiwa kwa ajili ya makazi mbadala katika kata ya Kibada. Kazi ya kupima na kuthamini mali katika maeneo hayo inaendelea kwa

kushirikiana na wananchi katika ngazi za Mitaa. Kamati za Mitaa za Wadau zimeundwa na wananchi wenyewe katika mitaa ya Uvumba na Kifurukwe. Pia, Wizara itaanzisha Mfuko wa *Kigamboni Investment Trust Fund*, ambao utawezesha wananchi wa Kigamboni kushiriki kama wanahisa katika uendelezaji wa mji wa Kigamboni. Vilevile, Wizara imeingia makubaliano (MOU) na kampuni mbili za nje kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi mbadala. Kampuni ya *Mi World* kutoka Dubai – Falme za Kiarabu inatarajiwa kujenga nyumba **5,000** na kampuni ya *China Hope Limited* kutoka China inatarajia kujenga nyumba **10,000**. Wananchi wa Kigamboni watakaolipwa fidia watapewa fursa ya kwanza kununua nyumba hizo kwa kutumia fidia hiyo moja kwa moja. Utaratibu huu wa kulipia nyumba mpya kwa kutumia fidia ndio unaotambuliwa na Umoja wa Mataifa kama mfano bora wa kuhamisha wananchi (best practice in resettlement schemes). Kumlundikia mtu malipo na kumtegemea ajenge nyumba mpya mwenyewe una mapungufu kwa sababu inamaanisha atafute eneo jipya na ajenge. Mchakatoa huu hupoteza muda na kusababisha fidia yake kupunguka thamani. **Ninachukua fursa hii kuwahimiza wananchi kutoa ushirikiano**

**katika mbinu hizi za kisasa kujiletea maendeleo endelevu.**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/14 Wizara itaendelea na kazi ya uendelezaji wa Mji Mpya Kigamboni kwa: kufanya uthamini wa mali na kulipa fidia kwa wananchi watakaotakiwa kupisha ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, majitaka na barabara kwenye awamu ya kwanza ya utekelezai wa Mpango. Aidha, Wizara itaendelea kuujengea uwezo Wakala ili uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuupatia wataalam na vitendea kazi. **Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru tena wananchi wa Kigamboni kwa ushirikiano wanaoendelea kutupa na ninawahakikishia kuwa Wizara itaendelea kuwashirikisha katika hatua zote za utekelezaji wa Mpango huu. Pia ninatambua mchango mkubwa na ushirikiano tuliopata kutoka kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke na Halmashauri nzima kwa uelewa na ushirikiano ambao umetuwezesha kuanzisha shughuli za KDA kwa pamoja.**

**Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji wa Miji na Vijiji**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2012/13 Wizara yangu imeendelea kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miji nchini kwa kupitia na kutoa vibali ambavyo vinazingatia mipango ya uendelezaji miji hususani ***zoning plans*** ili kuwepo na uwiano mzuri wa matumizi ya ardhi na majengo katika maeneo mbalimbali ya miji na kuwarahisishia waendelezaji/wajenzi kuandaa mipango yao. **Natoa wito kwa Halmashauri zote za miji kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye mipango ya uendelezaji miji katika utoaji wa vibali vya ujenzi mijini.**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) imefanya zoezi la kutambua maendelezo yaliyo ndani ya ukanda wa mita sitini wa ufukwe wa bahari ya Hindi katika eneo la Mbezi na Kawe jijini Dar-es-Salaam. Jumla ya viwanja **46** vilibainika kuendelezwa ndani ya ukanda huo na zoezi hilo bado linaendelea.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini itaendelea kusimamia

na kudhibiti uendelezaji wa Miji, kutoa elimu juu ya kanuni mpya za Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali. Vilevile taratibu za uanzishwaji wa Ofisi za Kanda za wataalamu wa Mipangomiji ili kukasimu Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mipangomiji zitakamilishwa baada ya taratibu za kurekebisha vifungu vya Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 kukamilika.

72. ***Mheshimiwa Spika*** kwa mwaka 2012/13 Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za jiji la Dar es Salaam kuhakikisha Askari Ardhi wanaendelea kufanya kazi ya ufuatiliaji wa ujenzi holela unaokiuka taratibu za Sheria ya Mipangomiji. Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa kibali cha kurejesha kada ya askari ardhi kwenye muundo wa utumishi wa umma.Aidha tayari Wizara ya Mambo ya Ndani imetoa kibali cha kuwa na *Auxiliary Police* na mawasiliano yanaendelea. Ni vyema Halmashauri zote nchini zikaharakisha mchakato wa kuajiri watumishi wa kada hii.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhifadhi Bonde la Mto Msimbazi kuwa eneo la kijani, Wizara yangu kwa mwaka 2012/13

imeshirikiana na Halmashauri za Ilala na Kinondoni na wadau wengine kubaini na kutambua maendelezo yaliyopo katika eneo lililotangazwa kuwa eneo la kijani. Rasimu ya awali ya awamu ya kwanza ya mpango (kuanzia eneo la daraja la Selander-Upanga hadi Vingunguti) lenye ukubwa wa hekta **1,121** inayoonesha hali halisi ya eneo hilo imeandaliwa. Kwa mwaka 2013/14 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri hizo itakamilisha rasimu ya Mpango na kuuwasilisha kwa wadau ili kupata maoni yao.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 wizara yangu ilitoa elimu ya mwongozo wa kupanga makazi ya vijiji nchini kwa wataalam wa sekta ya ardhi kwa Kanda ya Mashariki. Lengo la elimu hiyo ni kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji zikiwemo Halmashauri za Wilaya na Vijiji ili kupanga na kusimamia Mipango ya Makazi katika vitovu vya vijiji. Kwa mwaka 2013/14 Wizara itaendelea kutoa elimu ya Mwongozo wa kupanga makazi ya vijiji kwa wataalam na wadau wengine wa ardhi ya vijiji katika Kanda ya Kusini Magharibi ili kwenda sawia na programu ya *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* (*SAGCOT*). Vilevile, mchakato wa kuandaa Mwongozo wa

kusimamia ukuaji na uendelezaji wa Vituo vya Biashara (*Trading centres*) Vijijini ambavyo vinakua kwa vv kasi utaanza ili kuziwezesha mamlaka husika kusimamia uendelezaji wa vituo hivyo.

## MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

75. ***Mheshimiwa Spika***, Mipango ya Matumizi ya Ardhi ni nyenzo muhimu sana katika uendelezaji wa ardhi na rasilimali zake kwa ufanisi, kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi na kuimarisha milki za ardhi. Aidha mipango hii huwezesha wananchi vijijini kutenga kwa njia ya ushirikishwaji maeneo yanayotosha mahitaji yao na vizazi vyao kwa matumizi mbalimbali, kutenga maeneo kwa uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji na pia kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, hivyo kuongeza ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na jamii.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilitoa mafunzo kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa Sekretariati ya Mkoa

wa Morogoro na watendaji wa Halmashauri za Kilombero na Ulanga. Pia Tume ilitoa mafunzo kama hayo kwa watendaji wa Halmashauri za wilaya za Tarime  na Mkuranga. Aidha Tume iliendelea na uhamasishaji na kutoa elimu juu ya Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa wadau mbalimbali.

Pia  katika kipindi hiki Wizara kupitia Tume iliandaa Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007, na kuendesha warsha ya kupata  maoni ya wadau kuhusiana Kanuni hizi. Wadau walioshiriki ni wawakilishi wa Idara na Taasisi za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Vyuo Vikuu,  Sekta Binafsi, na Waandishi wa Habari.

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji**

77. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2012/13 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau mbalimbali kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Vijiji. Katika kipindi hiki jumla ya vijiji **111** katika Wilaya **15** viliandaliwa

mipango ya matumizi ya ardhi. **(Jedwali Na. 10).** Katika vijiji hivyo, maeneo ya matumizi mbalimbali ya ardhi yalitengwa kwa kushirikisha wananchi katika maeneo husika. Vile vile, Wizara kupitia Tume ilishirikiana na Halmashauri za Wilaya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji ambavyo vimeishaandaa mipango ya matumizi ya ardhi. Kwa mfano, katika wilaya ya Rufiji tathmini na ufuatiliaji ulifanyika katika vijiji 10, ambavyo wafugaji na mifugo walihamia.
Vile vile, katika kipindi hiki mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya nne za Kilombero, Ulanga, Muleba na Mpanda iliandaliwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara kupitia Tume itawezesha upangaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa ushirikishwaji katika vijiji **150** katika wilaya mbalimbali. Mipango hiyo itaandaliwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na Halmashauri za Wilaya hususan za mipakani mwa nchi na zile zenye migogoro sugu ya ardhi. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na wadau itawezesha kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya nne za Newala,

Tarime, Rorya na Maswa. Kazi hii itakwenda sambamba na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wilayani kuhusu mahudhui ya sheria za ardhi na mbinu shirikishi za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Aidha katika kipindi hiki, Wizara itakamilisha kuanda na kuchapisha Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007. Pia Tume itachapisha na kusambaza Toleo la Pili la Miongozo ya Ushirikishwaji katika Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini. Aidha, Tume itaendelea kutekeleza mradi wa SAGCOT kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kutenga maeneo yanayotosheleza mahitaji ya matumizi ya ardhi ya wananchi, kutenga maeneo kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji na ardhi inayofaa kwa uwekezaji.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** natumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri za Wilaya ambazo zilitenga fedha katika mwaka 2012/13 kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika maeneo yao. **Napenda kuendelea kusisitiza kwa Halmashauri za Wilaya nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi katika maeneo yao.**

## MAENDELEO YA NYUMBA

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua mchango wa sekta ya nyumba kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Pia, inatambua kwamba upatikanaji wa nyumba bora za bei nafuu ni moja ya kiashiria cha kukua kwa uchumi na kupungua kwa umaskini. Ubora wa nyumba na makazi kwa ujumla unachangia kuwepo kwa hali bora ya maisha kwa wananchi na hivyo kuchangia kuongezeka kwa tija na ufanisi katika shughuli za uzalishaji. Serikali inatambua pia kwamba sekta ya nyumba inachangia mapato ya Serikali, kuongezeka kwa nafasi za ajira, ongezeko la kipato cha mmiliki wa nyumba na hivyo kuchangia kukua kwa uchumi na kupungua kwa umasikini. Kwa kutambua hayo, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uendelezaji wa nyumba.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2012/13 niliainisha baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya nyumba kuwa ni pamoja na kupanda kwa gharama za ujenzi wa nyumba, kuwepo kwa miundombinu duni, huduma za jamii ambazo hazikidhi mahitaji katika maeneo ya makazi na riba kubwa katika mikopo ya nyumba. Aidha,

changamoto nyingine ni kipato kidogo wanachopata wananchi walio wengi ambacho hakiwawezeshi kumiliki au kuwa wapangaji kwenye nyumba zilizojengwa kwa viwango stahiki. Hata hivyo, tunafarijika tunaposhuhudia kushuka kwa mfumuko wa bei kutoka asilimia **19** mwaka jana hadi asilimia **10** kwa mwaka huu. Hii ni dalili nzuri inayoweza kuchangia kushuka kwa riba ya mikopo na gharama za vifaa vya ujenzi.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/14 Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu katika kuweka mifumo ya kifedha itakayowezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu. Aidha, tunashirikiana na Wizara na taasisi zingine ili kuweka mikakati ya kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba, upatikanaji wa ardhi na miundombinu ya msingi kwa lengo la kuwezesha ujenzi wa nyumba za gharama nafuu watakazomudu kununua au kupangisha wananchi walio wengi.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya nyumba, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa *Tanzania Mortgage Refinancing Company*, sasa itaaanza kukopesha benki hata kabla benki hizo

hazijatoa mikopo. Lengo ni kuyapatia mabenki mtaji wa kukopesha kwa muda mrefu. **Ninatoa wito kwa benki za biashara ambazo hazijaanza kutumia chombo hiki wakitumie na kutoa mikopo ya nyumba yenye riba nafuu kwa wananchi.**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inalo jukumu la kuweka mazingira yanayowezesha makundi mbalimbali kumiliki nyumba bora za gharama nafuu. Katika mwaka 2012/13 Wizara ilishirikiana na taasisi zingine za umma kuandaa mpango wa kuwawezesha watumishi wa umma kumiliki nyumba kwa kutumia mikopo itakayotolewa na benki za biashara kwa miaka hadi 25. Utekelezaji wa mpango huu utaanza mwaka 2013/14. Ili kuwezesha utekelezaji huo, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali utabadilishwa kuwa Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wote wa umma.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Wizara iliendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu kuandaa utaratibu wa mikopo midogo midogo ya kujenga nyumba (housing microfinance). Utaratibu huo unatarajiwa kuwasaidia wananchi walio wengi wanaotarajia kumiliki

nyumba na ambao hawawezi kumudu masharti ya kukopa kutoka benki ili nao waweze kupata mikopo midogo midogo ya kujenga au kukarabati nyumba hatua kwa hatua. Kwa mwaka 2013/14 Mfuko wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba utaanzishwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2012/13 Wizara ilikamilisha rasimu ya Sera ya Nyumba. Sera hiyo itakapokamilika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaandaa Mswada wa Sheria ya Nyumba ambayo inatarajiwa kutoa mwongozo na masharti ya uendelezaji wa nyumba hapa nchini.

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) una majukumu ya kutafiti, kukuza, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalamu wa ujenzi wa nyumba na za gharama nafuu nchini.
***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2012/13 Wizara kupitia Wakala iliendelea kufanya utafiti na kubuni mbinu za kujenga nyumba

kwa gharama nafuu kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Vilevile kazi za ushauri zilifanyika kwa wateja mbalimbali zikiwemo Ofisi za Serikali na watu binafsi. (**Jedwali Na. 11a**).

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Aprili, 2013 mashine **200** za tofali za kufungamana, kalibu (*moulds*) **150**, mashine za kutengeneza vigae (*tile vibrators*) **77** na mashine moja mpya ya kutengeneza aina mpya ya vigae zilitengenezwa katika maabara za NHBRA. Aidha, utafiti wa vifaa vya ujenzi ulifanyika katika maabara za Wakala pamoja na kuendesha Mafunzo kwa vitendo ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Wilaya za Tabora Mjini, Arusha Mjini na Vijijini, Kilwa, Biharamulo na Dodoma Mjini (**Jedwali Na. 11b**). Pia, Wakala ulisambaza matokeo ya tafiti kupitia maonesho mbalimbali ya kitaifa na katika vyombo mbalimbali vya habari.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti yangu ya mwaka 2012/13 Wizara iliahidi kuwa kupitia Wakala ingehamasisha na kueneza teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika wilaya za Arusha Vijijini, Nkasi, Kishapu, Chunya, Tandahimba na Muleba. Kazi hii ilifanyika katika wilaya ya Arusha vijijini na

wilaya zilizobaki zitafanyiwa uhamasishaji katika mwaka 2013/14. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na wilaya itaendelea kuimarisha vikundi vya ujenzi wa nyumba vilivyoanzishwa na kutangaza huduma zinazotolewa kupitia vyombo vya habari.

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

### Kuimarisha Utendaji kazi wa Shirika

90. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2012/13 Wizara iliendelea kulisimamia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika utekelezaji wa malengo ya Mpango Mkakati wake wa kipindi cha 2010/11-2014/15 ikiwa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi. Shirika liliendelea kuboresha muundo wake kwa kuwahamishia wataalam wa fani ya ujenzi mikoani ili kuongeza kasi na ufanisi katika utekelezaji wa miradi. Shirika pia liliweza kuwapatia mafunzo ya kitaaluma wafanyakazi wa ngazi za chini na baadaye kuwaongezea majukumu. Kadhalika, Shirika liliendelea kuboresha mfumo wa kupima na kutathimini utendaji wa kazi wa wafanyakazi kwa malengo ya majukumu yao; kuendelea kuimarisha

kitengo cha huduma kwa wateja; kuanzisha mfumo mpya wa kompyuta wa kusimamia rasilimali watu; na kutathmini uwiano wa wafanyakazi na majukumu yao ili kupata idadi inayolingana na mahitaji ya Shirika. Juhudi hizi, pamoja na kipindi cha televisheni cha Maisha ni Nyumba kinachoielimisha jamii kuhusu Shirika, ziliwezesha Shirika kuongeza ufanisi katika utendaji na kuboresha taswira yake kwa jamii.

**Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Ujenzi wa Nyumba**

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Shirika lililenga kuendelea na mchakato wa ununuzi wa ardhi yenye ukubwa wa ekari **26,887.9** katika Wilaya mbalimbali nchini. Lengo la ununuzi huu, ni kuliwezesha Shirika kuwa na hazina ya ardhi ya kutosha itakayoliwezesha kutekeleza jukumu lake jipya la kuwa mwendelezaji mkuu wa miliki. Hadi Aprili, 2013, Shirika lilifanikiwa kukamilisha ununuzi wa ardhi yenye ukubwa wa ekari **1,210.6** na viwanja **457** na liliendelea na mchakato wa ununuzi wa ardhi yenye ukubwa wa ekari **18,421** iliyoko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi (**Jedwali Na 12a**). Kwa mwaka 2013/14, Shirika litaendelea na

ununuzi wa ardhi ambao kwa sasa umefikia hatua mbalimbali.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Shirika liliweka lengo la kutayarisha miradi yenye jumla ya nyumba **9,000** za makazi na biashara. Matayarisho haya ambayo ni hatua ya kwanza katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi, yanahusisha upangaji na upimaji wa maeneo ya ardhi; utayarishaji wa michoro ya kiusanifu na kiuhandisi; upatikanaji wa vibali kutoka taasisi mbalimbali zikiwemo Baraza la Mazingira, Bodi ya Makandarasi, Halmashauri za Miji na Manispaa na Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC); pamoja na zabuni za kandarasi za ujenzi. Hadi Aprili, 2013, Shirika liliweza kutayarisha miradi yenye jumla ya nyumba **8,450** za makazi na biashara zitakazojengwa sehemu mbalimbali nchini.

93. ***Mheshimiwa Spika*** , katika mwaka 2012/13 Shirika la Nyumba la Taifa liliweka lengo la kuendelea kutekeleza miradi saba (**7**) yenye jumla ya nyumba za makazi **737** na kuanza utekelezaji wa miradi mingine yenye jumla ya nyumba za makazi **4,114** zikiwa ni za gharama nafuu, kati na juu. Hadi Aprili, 2013, Shirika liliendelea na utekelezaji wa miradi saba (**7)** ya ujenzi wa nyumba **564** za gharama ya kati na juu na kuanza miradi **11**

ya ujenzi wa nyumba **642** za gharama nafuu (**Jedwali Na. 12b)**. Katika utekelezaji wa miradi hii ya ujenzi Shirika limekutana na changamoto mbalimbali zikiwemo zile za kutopata kwa wakati ardhi huru kwenye Halmashauri za Miji pamoja na vibali vya ujenzi. Kwa mwaka 2013/14, Shirika litaendelea kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza miradi mingine mipya. Shirika litatoa kipaumbele kwa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zisizopungua **20** kwa kila mkoa. Lengo ni kufikia nyumba za gharama nafuu zisizopungua **5,000** ifikapo mwezi Juni, 2015.

94. ***Mheshimiwa Spika***, kulingana na Mpango Mkakati wa kipindi cha 2010/11 – 2014/15, Shirika linauza asilimia **70** ya nyumba za makazi zinazojengwa na kupangisha asilimia **30**. Hadi Aprili, 2013, Shirika liliweza kuuza nyumba **386** katika miradi yake. Kutokana na mauzo hayo, hadi Aprili, 2013 Shirika lilipata kiasi cha **Shilingi bilioni 23.3** kati ya **Shilingi bilioni 77.1** zinazotarajiwa wakati miradi hii itakapokamilika.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Shirika lilipanga kuanza utekelezaji wa miradi 14 ya majengo ya biashara. Hadi Aprili, 2013 Shirika liliweza kukamilisha mradi mmoja (1) wa ghorofa nne (4) ulioko Kigoma. Vilevile, Shirika lilianza ujenzi wa jengo la ghorofa 13 lililoko katika makutano ya Mtaa wa Ufukweni na Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Upanga - Dar es Salaam. Miradi mingine tisa (9) ilikuwa katika hatua mbalimbali za kuwapata makandarasi wa ujenzi. Aidha, Shirika lilikamilisha miradi mingine 11 iliyotekelezwa kwa ubia na sekta binafsi na kuendelea na ujenzi wa miradi mingine 20 ya ubia. Kwa mwaka 2013/14, Shirika litaendelea na utekelezaji wa miradi tisa (9) ya majengo makubwa ya biashara na majengo mengine 20 yanayojengwa kwa ubia. Pia, Shirika litaandaa mpango wa kina wa uendelezaji wa Kituo cha Huduma cha Luguruni ambao utahusisha sekta binafsi. Utekelezaji wa miradi hiyo unazingatia sera mpya ya uwekezaji inayoshirikisha sekta binafsi na kuboresha maslahi ya Shirika kwenye miradi hiyo.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13, Shirika liliendelea kutafuta mitaji

kwa ajili utekelezaji wa miradi ya ujenzi. Hadi Aprili, 2013 Shirika lilikuwa limefanikiwa kuingia mikataba ya mikopo ya kiasi cha **Shilingi bilioni 172**, na kuweza kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 92**. Shirika pia liliendelea na juhudi za kuwahamasisha wanunuzi wa nyumba zake watumie fursa ya mikopo inayotolewa na benki tisa (9) ambazo ni Azania Bank, Bank of Africa, CRDB - Bank, Exim Bank, KCB, NBC, Commercial Bank of Africa, NMB na Stanbic yaliyoingia makubaliano ya kutoa mikopo ya ununuzi wa nyumba. Wanunuzi wapatao 40 waliweza kupata mikopo kiasi cha **Shilingi bilioni 4.5** na wengine wanaendelea na mchakato wa kupata mikopo hiyo. Kwa mwaka 2013/14, Wizara kupitia Shirika itaendelea na juhudi za kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara.

**Mapato ya Shirika**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Shirika lilitarajia kuingiza mapato yatokanayo na kodi za pango la nyumba kiasi cha **Shilingi bilioni 52.97** na kuchangia **Shilingi bilioni 24.2** kama mapato ya Serikali. Hadi Aprili, 2013, mapato hayo

yalifikia **Shilingi bilioni 57.801** sawa na asilimia **131** ya lengo la kipindi hicho (**Jedwali Na. 12c**). Ongezeko hili, lilitokana na juhudi za kupandisha viwango vya kodi za pango kutoka asilimia **25** hadi **60** ya viwango vya soko kwa baadhi ya nyumba; juhudi za ukusanyaji; na makusanyo ya malimbikizo ya madeni. Mapato hayo, yaliliwezesha Shirika kuchangia mapato ya Serikali kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 11.81** kupitia kodi mbalimbali kama vile kodi ya pango la ardhi, kodi ya ongezeko la thamani, kodi ya majengo, kodi ya mapato, ushuru wa huduma za Halmashauri za Miji na Manispaa, kodi za mapato ya wafanyakazi na ushuru wa maendeleo ya taaluma (**Jedwali Na.12d).** Kwa mwaka 2013/14 Shirika linategemea kuingiza kiasi cha **Shilingi bilioni 63.2** kutokana na kodi za pango. Vilevile, Shirika litaendelea kuchangia mapato ya Serikali kupitia kodi mbalimbali.

## Matengenezo ya Nyumba na Majengo

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kupanda kwa viwango vya kodi pamoja na juhudi za ukusanyaji wa kodi hizo, kumeliwezesha Shirika kuzifanyia nyumba zake matengenezo makubwa na kwa wakati. Matengenezo kama

haya hayakuweza kufanyika huko nyuma kutokana na matatizo ya ufinyu wa mapato na kutokusanywa kodi kwa wakati. Hadi Aprili, 2013, Shirika lilitumia kiasi cha **Shilingi bilioni 7.4** kwa ajili ya matengenezo. Kwa mwaka 2013/14, Shirika litatenga kiasi cha **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa nyumba na majengo yake.

## HUDUMA ZA KISHERIA

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inacho Kitengo cha Sheria ambacho kilianzishwa mahususi kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali za kisheria katika Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Huduma za Kisheria zinajumuisha kutunga sheria mpya, kuhuisha sheria na kusimamia mashauri yanayohusu Wizara.

100. ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa lengo la kuhakikisha uwazi katika shughuli za uthamini na kuongeza weledi na uwajibikaji wa wataalam wa uthamini nchini, Wizara imeandaa na kuwasilisha rasimu ya Sheria ya Uthamini Serikalini. Kutungwa kwa Sheria hiyo kutawezesha uthamini nchini kufanyika kwa viwango vinavyokubalika kimataifa na watendaji watatekeleza kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoendana na misingi ya Kitaaluma. Kimsingi, sheria hii itawawezesha Wathamini kutambua majukumu yao, haki zao, wajibu wao na adhabu zitakazoweza kutolewa dhidi yao mara wanapokwenda kinyume na maadili ya kazi zao. Katika mwaka 2013/14 muswada huo utawasilishwa Bungeni baada ya kuridhiwa na Serikali.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2012/13 Wizara yangu vile vile imekamilisha marejeo ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007; Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334); Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117); Sheria ya Umilikaji sehemu ya Jengo, (Sura ya 416) na Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210) na kuwasilisha kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuandaa Muswada.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara yangu itaendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria ya Ardhi, sura ya 113; Sheria ya Ardhi ya Vijiji, sura ya 114; Sheria ya Mahakama za Ardhi, sura ya 216 na Sheria ya Wapima Ardhi, sura ya 324. Pia, Wizara itaendelea na mchakato wa kutunga upya Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sheria ya Maadili ya Maafisa Ardhi na Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki. **Natoa wito kwa wadau wa sekta ya ardhi kutoa maoni yao mara watakaposhirikishwa ili kuboresha sheria hizo.**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua athari za migogoro ya ardhi katika

suala zima la maendeleo na inafahamu kuwa sio kila mgogoro wa ardhi unaweza kutatuliwa kwa taratibu za mahakama, kwa msingi huo Wizara inatumia taratibu za kiutawala kutatua baadhi ya migogoro. Katika mwaka 2012/13 wizara imeweza kutatua migogoro mikubwa ya mipaka ya vijiji katika Wilaya ya Ngorongoro. Kamati maalumu imeundwa na itawezeshwa ili kuweza kutatua migogoro ambayo kwa sura yake haiwezi kutatuliwa mahakamani, hivyo kuhitaji njia za usuluhishi za kiutawala.

## MAWASILIANO SERIKALINI

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inaendelea kuhakikisha mawasiliano yanapewa umuhimu wa kutosha. Katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka wa fedha 2012/13 Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kimeendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika vipindi vya redio na luninga juu ya masuala ya Sera, mikakati utoaji huduma za sekta ya ardhi na uelimishaji wa sheria na kanuni zinazosimamia ardhi. Baadhi ya vipindi hivyo ni Haba na haba kinachorushwa na BBC kilichozungumzia changamoto na njia za utatuzi wa migogoro ya ardhi, Kipindi maalum kilichorushwa na Shirika

la Utangazaji nchini TBC kuhusu tathmini ya utoaji wa huduma za ardhi dhidi ya rushwa, Kipindi cha Kipimajoto na makala za uelimishaji wa dhana ya mji mpya wa Kigamboni kupitia magazeti. Aidha Wizara imeendelea kushiriki maonesho ya nane nane ambayo yanatoa fursa ya kukutana na kujadiliana na wadau wake ambapo mawazo yao husaidia kuboresha utendaji wa sekta ya ardhi.

Kwa mwaka wa fedha 2013/14 Wizara itakamilisha usimikaji wa mtandao rasmi wa kijamii (official ardhi blog) ambao utawahabarisha wadau wake kuhusu matukio mbalimbali ya sekta ya ardhi. Vile vile, Wizara itaendelea kuhuisha mkakati wa mawasilino pamoja na kuimarisha Kitengo cha Mawasiliano kwa kuongeza wataalam na vitendea kazi.

## HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU

105. ***Mheshimiwa*** **Spika,** Wizara yangu imeendelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa rasilimali watu kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi na kuongeza tija na ufanisi. Kwa mwaka 2012/13 Wizara

imeendelea kuimarisha utawala bora kwa watumishi kuzingatia maadili katika utendaji kazi, kuondokana na vitendo vya rushwa, kujali wateja na kutoa huduma kwa wakati.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2012/13 Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa kituo cha huduma kwa wateja. Kazi hiyo ipo katika hatua za mwisho. Kukamilika kwa kituo hiki kutaboresha utoaji wa huduma kwa ufanisi na uwazi. Kwa mwaka 2013/14 Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma, mazingira ya kazi, na kutoa stahili kwa watumishi kwa kuzingatia masharti ya ajira zao.

107. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo ya aina mbalimbali ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2012/13 jumla ya Watumishi **619** walihudhuria mafunzo kama ifuatavyo:- Mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi watumishi **52**, mafunzo yaliyohusu maadili katika utumishi wa umma watumishi **110** na mafunzo kuhusu mfumo wa wazi wa tathmini ya utendaji kazi (*OPRAS)* watumishi

**457 (Jedwali Na. 13a)**. Katika kipindi hicho watumishi **59** wa taaluma mbalimbali waliajiriwa, watumishi **200** walipandishwa vyeo na **13** walithibitishwa katika vyeo vyao. Kwa mwaka 2013/14 Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi **450.**

108. ***Mheshimiwa Spika***, ili kupambana na janga la UKIMWI katika sehemu ya kazi, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa kutumia utaratibu wa kuwaleta wizarani wataalam wa huduma ya ushauri nasaha na kupima kwa hiari. Wizara imekuwa ikiwapatia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI msaada wa dawa na lishe. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa michezo kwa afya za watumishi, Wizara ilishiriki katika mashindano ya SHIMIWI na kufanikiwa kupata tuzo mbalimbali. Kwa mwaka 2013/14 Wizara itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya na kuendelea kutoa huduma stahiki.

**Vyuo vya Ardhi**

109. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya Stashahada na Cheti katika fani za Usimamizi wa Ardhi, Uthamini na Usajili; Urasimu Ramani; Ubunifu

na Uchapaji; na Upimaji Ardhi. Fani hizi ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la mafundi sanifu wa sekta ya ardhí. Katika mwaka 2012/13 idadi ya wahitimu ilikuwa **240** kati yao **168** walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na **72** walitoka Chuo cha Ardhi Tabora **(Jedwali Na. 13b)**. Kwa mwaka 2013/14 Wizara itaendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. **Natoa wito kwa Halmashauri kuendelea kuajiri kada hii ya mafundi sanifu wanaohitimu katika vyuo hivi ili kupunguza uhaba uliopo.**

## SHUKRANI

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inashughulikia majukumu mbalimbali ambayo ni mtambuka. Ni mategemeo yangu kwamba, Bunge litaendelea kuwa na mtazamo chanya na kuipa kipaumbele sekta ya ardhi kwa ujumla ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio ya Wizara yangu yametokana na kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo zikiwemo taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani, taasisi zisizokuwa za

kiserikali na mashirika ya kidini. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-HABITAT), Shirika la Maendeleo la Ujerumani; na Serikali za Denmark, Sweden, Uholanzi na Uingereza kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara; na Serikali za Marekani, Finland na Norway.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bw. Patrick Rutabanzibwa, na Naibu Katibu Mkuu Bibi Maria Bilia kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Makamishna Wasaidizi na Wasajili Wasaidizi wa kanda, viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa sekta ya ardhi kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi. Naomba kila mmoja wetu aendelee kutekeleza majukumu yake kwa kujielekeza katika kuiwezesha ardhi kuwaondolea wananchi umaskini. Natambua kuwa Wizara yangu haina nyenzo na rasilimali za kutosha kutimiza matarajio ya Watanzania,

lakini hata kwa kutumia rasilimali chache zilizopo kwa uangalifu tutatoa mchango mkubwa kwa Taifa. Mwisho, namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa uchapisha Hotuba hii kwa wakati.

## HITIMISHO

113. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2013/14 Wizara imeazimia kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi, nyumba na makazi ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye kaulimbiu ya Kilimo Kwanza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Aidha, mbali na kuunda Wakala wa Kuendeleza Mji Mpya wa Kigamboni (KDA), Serikali itakamilisha uanzishaji wa chombo kitakachosimamia utoaji wa ardhi kwa wawekezaji kwa utaratibu mpya wa wananchi kutumia ardhi kama mtaji (*land for equity*). Vilevile, itahakikisha kuwa migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza inatafutiwa ufumbuzi na kuzuia migogoro mingine isitokee.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa hali hiyo Wizara imejipanga kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji na kuisimamia, kupanga matumizi ya ardhi, kupima ardhi,

kuhakiki milki, kusajili na kutoa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. **Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote ili kufikia malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.**

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2013/14

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imejipanga kutekeleza majukumu yake iliyojiwekea ili kufikia malengo ya MKUKUTA II, Dira ya Taifa ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 na Malengo ya Milenia. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | **Mapato**: | | |
| | • Mapato ya Serikali | Sh. | 100,048,261,480 |
| (ii) | **Matumizi ya Kawaida** | | |
| | • Matumizi ya mishahara | Sh. | 10,198,481,040 |
| | • Matumizi Mengineyo (OC) | Sh. | 25,959,443,000 |
| | **Jumla Shilingi** | **Sh.** | **36,157,924,040** |
| (iii) | **Matumizi ya Miradi ya Maendeleo** | | |
| | • Matumizi ya Maendeleo | | |
| | ○ Fedha za Ndani | Sh. | 56,172,349,000 |
| | ○ Fedha za Nje | Sh. | 16,000,000,000 |
| | **Jumla Shilingi** | | **72,172,349,000** |

Jumla ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 108,330, 273,040.**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara *www.ardhi.go.tz*.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.